# MAANA NA UMUHIMU WA UTAWALA BORA

***(Mada iliyoandaliwa kwa ajili ya Semina ya Madiwani, Januari 2006)***

## 1. Utangulizi:

Serikali imeweka umuhimu wa kwanza katika masuala ya Utawala Bora katika ngazi zote za uongozi wa Taifa letu kwa vile inaamini kuwa matatizo mengi yanayoisibu nchi hii yanatokana na kutozingatiwa kwa misingi ya Utawala Bora. Matatizo hayo ni pamoja na:

- Uongozi wa kiimla uinaoendelezwa na baadhi ya viongozi usiozingatia maoni na ridhaa ya walio wengi;
- Kutozingatiwa kwa sheria, kanuni na taratibu na miongozo ya kitaifa;
- Kutozingatiwa kikamilifu kwa misingi ya haki na usawa katika mipango na uendeshaji wa shughuli za umma;
- Kushamiri kwa vitendo vya wizi na ubadhirifu wa mali ya umma;
- Kushamiri kwa vitendo vya rushwa;
- Kushamiri kwa vitendo vya unyanyasaji wa wananchi;
- Kutokuwepo kwa uwazi katika uendeshaji wa shughuli za umma; na
- Kutokuwepo kwa utamaduni wa uwajibikaji kwa wananchi kutokana na maamuzi na vitendo vinavyofanywa na viongozi pamoja na wananchi.

Kwa kuzingatia matatizo hayo, Serikali imeweka na inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuwashirikisha kikamilifu wananchi katika kufanya na kutekeleza maamuzi yanayohusu ustawi na maendeleo yao. Mikakati hiyo ni pamoja na:

- Kuweka mwongozo wa kitaifa unaobainisha misingi ya Utawala Bora ikiwa ni pamoja na mipango inayochukuliwa kuimarisha utawala bora katika nyanja mbalimbali;
  - Marekebisho ya miundo ya Wizara za Kiserikali yenye lengo la kuziondolea majukumu ya kiutekelezaji na kubakia na majukumu ya kuandaa sera na kuratibu utekelezaji wa sera za kitaifa, kuweka mifumo ya kisheria, kuweka

na kufuatilia utekelezaji wa viwango vya kitaifa na kujenga mazingira yatakayoziwezesha Sekta Binafsi, na wananchi kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na utoaji wa huduma mbalimbali;

- Kuweka na kutekeleza mkakati wa kupeleka madaraka kwa wananchi unaotekelezwa kupitia Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa wenye lengo la kuongeza juhudi za kitaifa za kupunguza idadi ya wananchi walio katika hali ya umaskini. Kuziimarisha na kuziwezesha Serikali za Mitaa, ili, kwa kushirikiana na wadau wengine, ziweze kuboresha utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi na hasa kwa maskini.

Maelezo yafuatayo yanafafanua, angalau kwa kifupi, hali halisi ilivyo hivi sasa katika Halmashauri zetu:

**(a) Ubadhirifu:**

Kumekuwepo na malalamiko mengi ambayo yamethibitishwa na taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu matumizi mabaya ya fedha, watumishi na mali za Halmashauri zetu. Mara nyingi ubadhirifu juu umetokana na maamuzi mabaya ya Halmashauri zenyewe na mara nyingine kutokana na kutojali kwa watumishi wa Halmashauri zetu. Matokeo ya ubadhirifu huu yamekuwa yakidhoofisha Halmashauri husika; kudorora kwa huduma muhimu kwa wananchi na kupoteza imani ya wananchi kwa Serikali yao, na hivyo kususia wajibu wao wa kulipa kodi na kushiriki katika shughuli za maendeleo ya kijamii.

(b) **Rushwa:**

Sio jambo la siri kuwa rushwa imetanda na kushamiri katika Halmashauri zetu, hasa katika masuala yanayohusu utoaji wa huduma muhimu k.v. tiba, elimu, leseni za biashara, ugawaji wa viwanja, utoaji wa zabuni na ajira za watumishi. Vitendo vya rushwa vinafanyika wazi na bila aibu, na vinachukuliwa kama vitendo vya kawaida vinavyoendana na wakati. Matokeo yake ni wananchi kunyimwa haki zao za kimsingi, na kutokwa na imani na hata kuichukia kabisa Serikali yao. Kwa baadhi ya viongozi wetu

uongozi umegeuzwa kuwa biashara na sio utumishi kwa umma. Rushwa imechukuliwa kama kichocheo muhimu cha kujiimarisha kabla muda wa kuachia ngazi haujawadia.

(c) **Unyanyasaji wa Wananchi:**

Baadhi ya viongozi katika Halmashauri zetu wamepoteza dira ya uongozi bora. Badala yake wamekuwa wakitumia nafasi zao kuwakandamiza na kuwanyanyasa wananchi ili tu kuonyesha nguvu na uwezo wao bila kujali matokeo ya vitendo vyao kwa Serikali na kwa watu wasio na hatia. Vitendo hivi vinajitokeza waziwazi katika baadhi ya mbinu zinazotumika katika ukusanyaji wa kodi na aina nyingine za mapato, na pia katika utekelezaji wa Sheria Ndogo za Halmashauri zetu.

(d) **Huduma Duni:**

Kero nyingine ni ile inayohusu huduma duni zinazotolewa kwa wananchi kutokana na uzembe na kutojali kwa viongozi na watendaji. Licha ya kutambua hali ngumu ya kiuchumi na upungufu wa mapato, wananchi wanategemea viongozi wao kuhakikisha kuwa raslimali iliyopo inatumika kikamilifu katika utoaji wa huduma za msingi k.v. tiba, elimu, na huduma za maji na pia katika kuweka miundombinu itakayowawezesha kuimarisha shughuli zao za kiuchumi na maendeleo. Mara nyingi huduma muhimu na miundombinu vimeachwa kudorora, na hata kuharibika kabisa, hadi Serikali Kuu inapoingilia kati na kuwachukulia hatua wahusika kwa kutowajibika ipasavyo.

(e) **Kutojali Sheria na Taratibu Zilizowekwa:**

Sheria na taratibu mbalimbali zimewekwa ili kuongeza shughuli za Halmashauri zetu; kulinda haki za msingi za wananchi na kudhibiti vitendo visivyotakiwa au kukubalika katika jamii. Licha ya ukweli huo, umezuka mtindo ambamo baadhi ya viongozi na watumishi katika Halmashauri zetu hawajali sheria wala taratibu zilizopo. Kuna mifano mingi kuhusu jambo hili: kuvuruga kwa makusudi mipango ya matumizi ya ardhi katika sehemu za miji; kuruhusu biashara kuendeshwa kiholela, kutumia fedha bila kujali taratibu na kanuni za fedha n.k. Mtindo unaoonekana kupendwa sana na baadhi ya viongozi wa ngazi mbalimbali, ni ule

wa kutoa maagizo ya mara kwa mara kutaka hili au lile lifanyike katika muda wanaoutaka bila kujihakikishia kwanza kama sheria na taratibu zilizopo zinaruhusu na kama maagizo hayo kweli yana maslahi kwa wananchi.

(f) **Kutowajibika:**

Suala la uwajibikaji limekuwa linazungumzwa zaidi kuliko kutekelezwa. Fikra zilizotanda kwa walio wengi ni kwamba wanaopaswa kuwajibika kutokana na matokeo ya utendaji wao ni watumishi peke yao. Utaratibu wa viongozi kutoa taarifa kwa wapiga kura wao kuhusu utendaji wao ni jambo la nadra sana, na kwa wengi halipo kabisa. Pia si jambo la kawaida kuona kiongozi kwa hiari yake akikubali kuwajibika kwa maamuzi yake ambayo yameleta madhara makubwa kwa wananchi. Kinachoonekana zaidi ni utetezi usio na mwisho wala msingi wowote pindi wananchi wenyewe wanapoamua kuchukua hatua.

(g) **Kutowashirikisha Wananchi:**

Maamuzi mengi yanafanywa na Halmashauri yanapowagusa moja kwa moja bila kwanza kupata maoni yao. Tumeendeleza mno utawala msonge ambapo viongozi wamegeuka kuwa mabwana wenye kutoa amri na kufuatilia utekelezaji wake kwa nguvu zote. Kwa upande mwingine, Halmashauri zetu zimeendelea kubeba jukumu lote la utoaji wa huduma muhimu, na pia kubuni na kutekeleza mipango yote ya maendeleo katika sehemu zao. Wananchi wamebaki kuwa watazamaji na watumiaji tu wa huduma zinazotolewa, hali ambayo imewadumaza na hivyo kuchelewesha maendeleo yao wakati wakingoja Halmashauri ziwafanyie kila kitu.

Matokeo ya kutowashirikisha wananchi katika masuala yanayohusu ustawi na maendeleo yao, ni kuongezeka kwa malalamiko yao na kurudisha nyuma jitihada ya kuwa na maendeleo yanayohimili (endelevu).

## 2. Dhana na Misingi ya Utawala Bora

Utawala Bora ni dhana inayosimama katika msingi mkuu wa Ujumuishaji na Ushirikishwaji wa wahusika wote walio nadni ya jamii katika **maamuzi** na

utekelezaji wa maaumzi yanyohusu ustawi na maendeleo yao, kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa, uwazi na uwajibikaji. Utawala Bora ni nyenzo kuu na pia ni mhimili kwa maendeleo ya nchi yetu kisiasa, kiuchumi na kijamii. Nchi yetu imedhamiria kujenga Utawala Bora unaozingatia misingi ifuatayo:

(a) **Demokrasia:**

Demokrasia ni utaratibu ambamo viongozi wa wananchi hupatikana kwa njia ya uchaguzi unaoendeshwa kwa njia ya haki inayompa wnanchi uhusu wa kuchagua kiongozi anayemtaka.

Miongoni mwa taratibu zinazopaswa kufuatwa katika kudumisha demokrasia ya kweli ni pamoja na watu kujijengea utamaduni wa:

- Uvumilivu na staha kwa mitazamo na maoni tofauti ya kisiasa;
- Kufuata na kuheshimu mawazo ya walio wengi;
- Kutumia nguvu ya hoja na siyo hoja ya nguvu;
- Kupingana bila kupigana; na
- Kujikosoa na kukosoana bila kuleana.

(b) **Utawala wa Sheria:**

Katika utawala wa sheria kila mtu anapaswa kuzingatia na kuongozwa na Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo katika maisha yake mwenyewe, katika uhusiano na wengine na katika utekelezaji wa majukumu yake. Kiongozi hatarajiwi kupuuza au kujiweka juu ya sheria, maamuzi au maelekezo halali yaliyopo au kufanya kitendo chochote kinyume cha Katiba ama nje ya sheria. Matendo kama hayo ni batili na yanaweza kumfanya mhusika kuchukuliwa hatua za kisheria.

(c) **Haki na Usawa:**

Kiongozi anatakiwa kufanya maamuzi na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia haki, bila ubaguzi wala upendeleo wa aina yoyote ile. Kwa kufanya hivyo kiongozi atajenga moyo wa imani kwa wananchi na itakuwa rahisi zaidi kwake kupata ushirikiano wao katika harakati za maendeleo, na

pia katika vita dhidi ya umaskini. Ni muhimu sana kwa kiongozi khakikisha kuwa haki za akina mama, watoto, wazee, na wasiojiweza zinazingatiwa na kulindwa wakati wote.

(d) **Ushirikishwaji wa Wananchi:**

Maendeleo endelevu ya watu huletwa na watu wenyewe na wala hayaletwi na viongozi wala wafadhili. Viongozi wanatakiwa wawashirikishe wananchi katika maamuzi yote yanayohusu ustawi na maendeleo yao. Viongozi watatekeleza jukumu hili kwa kuitisha mikutano ya wakazi wote wa mitaa, vijiji na vitongoji kama inavyoelekezwa katika sheria, kanuni na miongozo iliyopo, yaani:

- Mkutano wa wakazi wote wa mtaa mara moja moja kila baada ya miezi miwili;
- Mkutano wa wakazi wote wa kitongoji, mara moja kila mwezi; na
- Mkutano wa wakazi wote wa kijiji mara moja kila baada ya miezi mitatu.

(e) **Uwajibikaji na Uwazi:**

Viongozi pamoja na watumishi wa Halmashauri katika ngazi zote, wapo kuwahudumia wananchi na sio kuwatawala au kuwaburuza. Viongozi wanaochaguliwa na wananchi wanatarajiwa kuwa karibu na wananchi wakati wote na wanapaswa kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu maamuzi pamoja na utendaji wao. Taarifa hizo zitawawezesha wananchi kupima na kuamua kama wanatekeleza wajibu wao kadri inavyotakiwa au la. Hali kadhalika maamuzi na vitendo vyote vya viongozi katika utekelezaji wa majukumu yao lazima vifanywe bila kificho ili wananchi watambue kinachoendelea.

## 3. Utekelezaji wa Dira ya Utawala Bora:

Serikali imeandaa na imekwisha kutekeleza mikakati mbalimbali ya Utawala Bora nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na marekebisho ya sheria, mifumo na taratibu zisnazoweka mtazamo mpya wa mahusiano kati ya raia na serikali kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; na kati ya ngazi mbalimbali za serikali, yenye lengo la

kusimika Utawala Bora kama njia muhimu ya kuharakisha maendeleo na kukabiliana na umaskini. Mikakati hiyo ni pamoja na:

- Kuziimarisha Serikali za Mitaa na vikundi vya kijamii na kupeleka madaraka na uwezo kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa;
- Kurekebisha miundo ya Wizara za Kisekta ili kuziwezesha wizara hizo kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi;
- Kuandaa mikakati ya kupambana na vitendo viovu vinavyojitokeza katika sekta ya umma k.v. rushwa, hongo, ubadhirifu n.k;
- Kuandaa mikakati ya jinsi ya kuwashirikisha wananchi katika shughuli zote za kiutawala, kiuchumi na za kijamii kupitia ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa;
- Kuweka taratibu za uwajibikaji, uwazi na ukweli katika uendeshaji wa shughuli za umma;
- Kuweka misingi imara ya Utawala wa sheria;
- Kuimarisha demokrasia ya Uchaguzi;
- Kuweka utaratibu imara unaolinda haki za msingi za raia;
- Kuboresha utoaji wa huduma za umma.

Mikakati hii inagawanyika katika maeneo makubwa matatu:

– Maeneo ya kisiasa;
– Maeneo ya kiuchumi; na
– Maeneo ya kiutendaji.

Mgawanyo huo unaonyesha pia mwingiliano mkubwa uliopo kati ya shughuli za maendeleo na Utawala Bora, kwa vile Utawala (Governance) hauchukuliwi tena kama jambo linalohusu Serikali tu, bali ni jambo linalowajumlisha wahusika wengine katika sekta binafsi na sekta ya jamii. Hii ina maana kuwa kila sekta ina haja ya kudhihirisha sifa zinazoendana na Utawala Bora na kwamba hatua za kuimarisha Utawala Bora nchini itabidi zihusu Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na pia sekta binafsi.

## 4. Mpango wa Uboreshaji wa Serikali za Mitaa

Serikali za Mitaa ni sehemu ya msingi ya madaraka ya Umma kwa vile ni Taasisi zinazowezesha wananchi kujitawala wenyewe na pia kubuni, kutekeleza, kusimamia na kudhibiti shughuli zinazohusu ustawi na maendeleo yao.

Mpango wa Uboreshaji wa Serikali za Mitaa ambao umeshaanza kutekelezwa, una shabaha ya kuziimarisha Serikali zetu za Mitaa ili ziweze kutoa huduma bora zaidi kwa kushirikiana na wahusika katika sekta mbalimbali pamoja na wananchi kwa ujumla. Misingi inayoongoza Uboreshaji wa Serikali zetu za Mitaa ni ile inayosisitiza katika uimarishaji wa Utawala Bora. Hii ni kwa vile penye Utawala Bora unakuwepo uhusiano na ushirikiano mzuri kati ya Serikali na wananchi katika shughuli za maendeleo ya uchumi.

Taswira ya kitaifa kuhusu mfumo mpya wa Serikali za Mitaa ni kuwa na Serikali za Mitaa ambazo kwa hakika, na kwa vitendo, zitawashirikisha wananchi katika kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo katika sehemu zao, na pia kuwa na Serikali za Mitaa ambazo zitaimarisha demokrasia katika maeneo yao na kuitumia demokrasia kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Yafuatayo ni baadhi ya maeneo muhimu yanayotiliwa mkazo katika uimarishaji wa Utawala Bora kwenye Halmashauri zetu:

### 1. Kuimarisha Utawala wa Kidemokrasia

Kuhakikisha kuwa Viongozi katika ngazi zote za utawala wanapatikana kupitia uchaguzi unaofanyika kwa kuzingatia misingi ya uhuru na haki. Vyama vya Siasa vikishirikiana na vyombo vya kiserikali, Taasisi zisizo za kiserikali na vikundi mbalimbali vya wananchi vitajihusisha kikamilifu katika kuwahamasisha wananchi kushiriki katika chaguzi za viongozi wa ngazi zote.

**2. Kupeleka Madaraka na Majukumu zaidi kwa Serikali za Mitaa na Ngazi za Chini za Serikali za Mitaa**

Madaraka, majukumu na raslimali zaidi zitaendelea kupelekwa kutoka Serikali Kuu kwenda kwa Serikali za Mitaa nkutoka ngazi za juu za Serikali za Mitaa hadi ngazi za chini za Serikali hizo ili kuwawezesha wananchi kushiriki kwa ukaribu zaidi katika kupanga, kutekeleza na kusimamia shughuli zinazohusu maendeleo yao; kuboresha ukuaji wa uchumi vijijini na mijini.

**3. Kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji**

Viongozi na watumishi wa Halmashauri wapo kuwahudumia wananchi na sio kuwatawala na kuwaburuza. Katika maboresho yanayoendelea kutekelezwa, suala la uwajibikaji limepewa uzito mkubwa pamoja na nguvu ya kisheria. Mbali ya taarifa za utendaji ambazo zitaendelea kutolewa Serikalini, viongozi wa kisiasa na watendaji watalazimika kuwa karibu zaidi na wananchi na kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa mipango na shughuli za Halmashauri zao zitakazowawezesha wananchi kupima na kuamua kama wanatekeleza wajibu wao kadri inavyotakiwa.

**4. Haki na Heshima kwa Wananchi**

Ili kuhakikisha kuwa viongozi wanawatendea haki na kuwaenzi wananchi kanuni za Maadili ya Madiwani na watumishi wa Halmashauri zinatungwa na zinatumika katika Halmashauri zote. Pamoja na mambo mengine, Kanuni hizo zinasisitiza masuala yanayohusu utoaji wa haki sawa kwa wote na uaminifu na ukweli katika utendaji wa shughuli za umma.

**5. Kupiga Vita Rushwa**

Rushwa ni dosari kubwa katika jamii na wala haiendi pamoja na Utawala Bora. Kila Halmashauri inatakiwa kuwashirikisha wananchi pamoja na wadau wote wa eneo la Halmashauri katika kubaini mazingira na sababu zinazosababisha rushwa katika maeneo yao; kuweka mikakati madhubuti ya

kupambana na rushwa na kuandaa na kutekeleza mipango ya utekelezaji ya kupambana na rushwa.

## 6. Utawala wa Sheria

Serikali za Mitaa ni vyombo vinavyotawaliwa na kuendesha shughuli zao kwa misingi ya sheria. Maamuzi, maagizo, maelekezo na vitendo vyote vya Halmashauri yenyewe, Diwani na mtumishi wa Halmashauri inabidi viendane na sheria na taratibu zilizopo. Wananchi wataelimishwa kikamilifu kuhusu haki na wajibu wao kama raia, na pia wajibu na uwezo wa viongozi wao ili waweze kuchukua hatua zinazotakiwa pale wanapoona kuwa vitendo vya viongozi na watumishi wa Halmashauri zao vimekiuka sheria.

## Mwisho

Kama ilivyooneshwa, Utawala Bora ni nyenzo muhimu ya kusukuma maendeleo ya wananchi mbele. Utawala Bora unaweza kusaidia sana katika kupunguza umaskini kutokana na wananchi wa aina zote kushiriki katika mchakato wa upangaji mipango ya uchumi wao na rasilimali kutumiwa vizuri. Hata hivyo, ni muhimu sana kwa viongozi wa Halmashauri kuzitumia sheria ndogo za Halmashauri, hasa zile zihusuzo kuinua uchumi wa wananchi, kusukuma watu wavivu ili nao washiriki katika kuzalisha mali ya kuwakomboa ama kuondokana au kupunguza umaskini.

Ili kujenga Utawala Bora ni muhimu kila Halmashauri ipange na kutekeleza haraka utaratibu wa kuwaelimisha wananchi juu ya haki na wajibu wao, na washauriwe na kuhamasishwa katika kudai haki zao na wao wenyewe kutimiza wajibu wao.

Kwa upande wa viongozi na watumishi wa Halmashauri, ni muhimu watambue kuwa wote ni watumishi wa umma katika nyadhifa tofauti. hivyo, ni lazima wawaheshimu wananchi ambao ndio wamewaweka madarakani. Ni lazima viongozi na watumishi wa Halmashauri wawe wasikivu kwa matakwa halali ya wananchi, na kuyafanyia kazi na kutoa taarifa za utekelezaji kuonesha jinsi

Halmashauri inavyoshughulikia matakwa yao na shida mbalimbali zinazowaandama.

Hayo yakitendeka, mahusiano ya Halmashauri na wananchi yataboreka na wananchi wakitambua kuwa viongozi wanatambua na kukubali kuwa chombo (Halmashauri) ni cha wananchi wananchi watakuwa tayari kukiunga mkono chombo chao na hapo Halmashauri itakuwa katika njia nzuri ya kushirikiana na wananchi kuleta maendeleo.